# MOUNT KENYA UNIVERSITY

## (VIRTUAL CAMPUS NAIROBI)

## BEC 3102

## (E-LEARNING NOTES).

**UTANGULIZI.**

Lugha yoyote ile ni lazima ipanuke ili iweze kukidhi mahitaji ya kila siku ya jamii husika .Kupanuka tunakorejelea ni kuongezeka kwa maneno katika lugha husika.Kama lugha haitaunda maneno kwa kasi inayohitajika huenda "ife".Watalaamu wa lugha(wanaisimu) huchunguza utaritibu unaotuniwa na lugha kujiongezea maneno.Wanaisimu huichunguza lugha katika viwango mbalimali;sauti,maneno,sentensi,maana,matumizi na hata diskosi.Kazi hii itajikita katika kiwango cha maneno(mofolojia)na sentensi(sintaksia).Viwango vingine vitashughulikiwa katika sehemu zingine za msululu wa vitengo vya kozi hii.Hata hivyo kwa yeyote ambaye angetaka kumakinika katika nyanja hii ni lazima aichukulie kazi hii kama mwongozo tu.Mpenzi yeyote wa lugha hii itamlazimu kusoma vitabu vingi na vya kisasa vilivyoandikwa na watalaamu wa lugha hii.Mwisho wa kazi hii pana baadhi ya marejeleo hayo.

**Madhumuni ya somo.**

(1) Kueleza istilahi mbalimbali zinazotumika kuelezea muundo wa Kiswahili kama vile  za kimofolojia,na kisintaksia.
(2) Kuelezea muundo wa sentensi ya Kiswahili.
(3) Kuchanganua sentensi ya Kiswahili kwa kutumia mitindo mbalimbali.

## Yaliyomo

**Sura ya kwanza**.

Ukurasa.

(a) Dhana ya mofolojia………………………………………………...….1
(b) Mofolojia ambishi na nominishaji…………………………………….2
(c) Uainishaji wa lugha kimofolojia……………………………………....2
(d) Dhana za kimofolojia ;mofu,mofimu,alomofu na leksimu………………....4
**(e)** Maswali………………………………………………………………11

**Sura ya pili.**

(a) Aina za maneno ya Kiswahili kama vile;nomino(N),viwakilishi(W),vivumishI(V),vitenzi(T),vihusishi(H), vihisishi(I) na viunganishi(U),……………………………………………..13
(b) Ngeli za nomino kwa kutumia mtindo wa isebati na viambishi vya nomino………………......... …………………………………………….21
(c) Nngeli za nomino kwa kufuata upatanisho wa kisarufi…………………..…26
(d) Dhana ya kiambishi…………………………………………….......29
(e) Aina za viambishi na dhana ya mzizi na shina…………………….....29
(f) Uundaji wa maneno…………………………………………………...32
(g) Maswali……………………………………………………………..31

**Sura ya tatu.** Ukurasa

(a) Sintaksia ya Kiswahili ………………………………………………..42
(b) Sarufi miundo virai……………………………………………………42
(c) Vipashio vya sentensi…………………………………………………43
(d) Aina za virai…………………………………………………………...44
(e) Upambanuzi wa tungo…………………………………………….....46
(f) Vishazi……………………………………………………………......48
(g) Aina za sentensi katika lugha ya Kiswahili………………………….....50
(h) Maswali…………………………………………………………….….57

**Vifupisho.**
Alama.

{ } alama zinazoashiria mofimu.
[ ]  huonyenyesha alama za kifonetiki.
/ /  huashiria fonimu.
Φ  kapa(kudondosha).
+  kuonyesha sifa iliyopo kwenye kipashio fulani.

## SURA YA KWANZA.

### Dhana ya mofolojia.

Wanaisimu kama vile Mathews (1974), Hartman (1972), Richard et al (1985) wamejaribu kufafanua dhana ya mofolojia.Habwe na Karanja(2004),wamejaribu kuelezea dhana ya mofolojia kwa kuyatafsiri mawazo ya Kiingereza kwa Kiswahili.Neno hili limetokana na neno la Kiingereza,morphology.Neno hili linatumika katika fani zingine lakini huwa na maana tofauti na vile ilivyo katika isimu.Fani hizo ni kama vile Jiografia,Sayansi ya Mimea na Utabibu wa Binadamu.

Ni vizuri tuangalie maoni ya wanaisinu mbalimbali kabla ya kutoa maoni ya jumla.

Kwa mujibu wa Mathews (1974),Mofolojia ni utanzu wa isimu uchunguzao maumbo ya maneno hasa maumbo ya mofimu.Kamusi ya Isimu na Lugha (1990), inaeleza Mofolojia kuwa tawi la isimu(utanzu) linalochunguza maumbo ya maneno na aina za maneno.Mchunguzi Hartman anakubaliana na maoni haya lakini anaongeza kipengele cha historia kwa kusema; Mofolojia ni tawi la isimu linaloshughulikia kuchunguza na kuchambua maumbo,fani,na aina za maneno yaliyopo sasa pamoja na historia yake.

Maelezo yoyote kati ya haya, kuhusu dhana ya mofolojia yatatosheleza somo hili.

Mofolojia hupatikana katika tanzu(matawi) mbili kuu;Mofolojia ambishi na nominishaji.

a) **Mofolojia ambishi**.Neno hili (ambishi) katika muktadha wetu lina maana ya kuongezea mofimu kwenye neno.(Tutaangalia maana ya mofimu hapo baadaye) Mofolojia ambishi huongeza maana ya kisarufi kwenye neno lakini haivushi neno kutoka aina moja hadi nyingine.Hivyo ni kusema hata neno likinyambuliwa(likiongezwa viambishi vya aina fulani litabaki aina iyo hiyo)kile kitakachoimarika ni upatanisho wa kisarufi tu.Kama lilikuwa kitenzi litabaki vivyo hivyo.

Mfano wa mnyambuliko;

| Mzizi/shina | Maneno yaliyonyambuliwa. |
|---|---|
| ukulima(nomino)<br>lima(kitenzi) | ukulima,kilomo(nomino)<br>limia,limiana(vitenzi) |

Kwa kuzingatia mfano katika jedwali;mnyambuliko huu haubadilishi aina ya neno.(kitenzi hubaki kitenzi na nomino hubaki nomino)

b) **Mofolojia nomonishaji** (mofolojia ya uundaji maneno mapya)

- Viambishi huongezwa kwenya mzizi na tunapata neno jipya kabisa .

  Mfano:

| **Vitenzi** | **Nomino** |
|---|---|
| cheza | mchezo, mchezaji, uchezaji, mchezewa |
| -refu | refusha |

**Uainishaji wa lugha kimofolojia**.

Kwa kutumia kigezo cha kimofolojia, lugha za ulimwengu zinaweza kugawa katika makundi matau makuu.Lugha;tenganishi,ambishi na changamano**.**

a) Tenganishi

Mfano mzuri wa lugha tenganishi ni lugha ya Kichina.Katika lugha hii mofimu moja ni neno moja zima.Mfano

| **Kichina.** | **Maana.** |
| --- | --- |
| Wo | Mimi (umoja). |
| wo men | sisi(wingi) |

Katika mfano huu ‘wo’ ni umoja (mimi) na ‘men’ni mofimu inayojisimamia ya wingi.

Kiingereza pia huwa sifa hii kwa kiwango fulani.

go-went

b) Lugha ambishi.

Katika lugha hizi viambishi hubainika(huonekana wazi)

Mzizi wa neno huwa haubadiliki hata neno likinyambuliwa.Kila kiambishi hubeba maana fulani.Mzizi wa neno katika lugha hizi unaweza kuwa na viambishi awali,kati na mwisho. Mf: Kiswahili, Kijapani, Kifini na Kituruki.

Mfano wa neno {m} {mchez} {o}

{m} ni kianbishi cha unominishaji .{o} ni kiishio.

c) Ambishi mchanganyo.

Hizi ni lugha ambazo hupenyezwa viambishi ndani ya mzizi wa neno wakati wa uundaji wa maneno mbalimbali – huwezi kutenganisha viambishi na mzizi kwa urahisi. Mfano: Kigriki, Kilatini na Kiarabu.

Mfano katika Kiarabu-{ktb} huu ni mzizi wa kitenzi (kuandika).Katika hali ya wakati uliopita kitenzi kitakuwa{kataba}. Mofimu /a/ imepenyezwa katikati ya kosonanti za mzizi wa kitenzi ili kupata hali ya wakati uliopita.

Lugha ya Kiingereza pia ina sifa hii. Mfano

come - came

(Katika vitenzi hivi hali ya wakati uliopita inaafikiwa kwa kuchopeka viambishi ndani ya mzizi au shina)

**Dhana za kimofoljia**;

a) mofu.

Mofu - Hudhihirisha mofimu kama vile foni hudhihirisha fonimu. Mofu ni yale maumbo halisi yanayozua mojimu. Mf: katika: Kiingereza:

chair -Ni umoja na'chairs' ni wingi.

chair - Ni mofu moja inayozua mofimu ya kileksia(maana ya kamusi)

chairs - Ni mofu mbili; moja inazua mofimu ya kileksia (chair) na mofimu ya pili ni kiambishi cha wingi (s)

b) mofimu.

Wanaisimu wengi wametoa ufafanunuzi wa dhana ya mofimu mmoja wao ni Hockett (1988), anasema ni tamko nndogo lenye maana.Kwa hivyo kulingana naye mofimu yaweza kuwa neno moja au sehemu ya neno.

Mofimu tunaweza kusema pia ni kipashio kindogo cha kisarufi kilicho na maana.

Hebu tujaribu kubainisha sifa mbalimbali za mofimu;

i. Mofimu ina umbo halisi.(foni)

ii. Ina umbo la kifonetiki.(sauti)

iii. Huwa na maana.(semantiki)

iv. Ina nafasi kisintaksia(mpangilio wa maneno katika sentensi) kuunda vipashio vikubwa vya kisarufi. Mf:

Neno mototo lina mofimu {m} + {toto}

{m} – mofimu ya ngeli /1/

{toto} – mzizi

Anasema:

| | | |
|---|---|---|
| {a} | - | nafsi |
| {-na-} | - | wakati |
| {som} | - | mzizi |
| {a} | - | kiishio |

**Mofimu mbalimbali.**

a) Mofimu huru.

Mofimu hizi hujisimania kimaana hazihitaji kuambatanishwa na viambishi vingine ili kuleta maana.Huwezi kuzigawa katika sehemu mbalimbali.Ukizigawa sehemu hizo hazitakuwa na maana.

- Mfano: kalamu, paka, taa.

Mofimu huru huwa ni za aina mbili; za kileksia na kiuwamilifu

i. za kileksia.

Mofimu za kileksia huwa ni maneno ya kawaida pamoja na vivumishi.Hizi ndizo hubeba maana kuu/ujumbe katika sentensi. Mf: Uganda,Ujerumani,dada n.k.

ii. za kiuwamilifu.

Hutenda kazi fulani katika lugha, mf: viungamishi vihusishi, vielezi n.k.

Mifano ya mofimu za kiuwamilifu;

- Viunganishi – lakini, aidha, bila, ilhali.
- Vihusishi – nje, ndani, juu, pekee, kwa.
- Vielezi – sana, leo, saa, tatu.

Mofimu huru ni maneno halisi.

b) Mofimu funge.

Haijitoshelezi kimaana bila viziada; huambatanishwa na viambishi vingine ili kuleta maana kamili. Mfano: Kiambishi cha ngeli ya kwanza (umoja)/m/katika neno mtu. /m/ kiambishi hiki hakina maana kama hakitaunganishwa na mzizi /-tu/.

Mofimu funge pia huitwa mofinu tegemezi kwa kutojisimamia kimaana.

Aina za mofimu funge (makundi ya mofimu funge):-

i. Mofimu ambishi.

Hivi ni viambishi ambavyo havijasimamii na havibadilishi mzizi wa neno; hupatikana mwanzoni, kati na mwishoni mwa neno.

ii. Mofimu nominishaji

Hutumiwa kuunda maneno mapya ambayo huwa katika kikundi tofauti na maneno asilia: mfano:

| **Kitenzi** | **Nomino** |
|---|---|
| kimbia<br>soma | mkimbiaji,mkimbizi,ukimbizi<br>somo,msomaji,usomaji,kusoma |

Kwa kuongeza kiambishi awli au tamati neno jipya linabuniwa mfano;kitenzi kinakuwa nomino.

c) Mofimu tata(vitate).

Hizi ni mofimu zenye maana zaidi ya moja licha ya kuwa umbo moja;

kaa, mbuzi,somo,

d) Mofimu changamano.

Mofimu changamano huundwa kwa kuweka pamoja mashina au mizizi .

miwili ya maneno ambayo kwa kawaida huwa huru. Maana ya ambayo hupatikana ni tofauti kabisa na ile asilia ya kila mzizi.Mf

mwana + siasa

mwana + habari

e) Mofimu kapa;

Hizi ni mofimu ambazo ni za kidhahamia (hazidhihiriki) yaani hazionekani kwa macho katika neno,haziandikwi wala kutamkwa.Hata hivyo athari zake zipo na hueleweka.

Mfano: ngeli ya 9/10 mf: nguo, samaki – huwa na mofimu kapa.

Pia ngeli ya 5/6 (ji-ma) –maneno debe na kasha; huwa na mofimu kapa katika umoja na wingi.

f) Mofimu mzizi.

Hii ni sehemu ya neno ambayo haibadiliki na hubeba maana ya kimsingi ya neno.Mfano; andika-andik-, soma-som-,cheza-chez.Mofimu hizi huambatanishwa na zingine ili kutoa maana(unyumbuaji).

Kwa mfano. mzizi andik- ukiongezwa kiambishi –ika ili kuwa andikika mzizi –andik haubadiliki.

**Vigezo vya kutambua mofimu.**

Habwe na Karanja(2004),wanatumia vigezo viwili vikuu katika kuainisha mofimu; maana au mofimu inayobebwa na mofu na,maumbo ya mofu zinazohusika.Lakini mwanaisimu Nida (1949) alipendekeza kanuni zifuatazo katika kutambua mofimu;

i. Maumbo yanayofanana kifonetiki na kisematiki yanabainishwa kama mofimu moja.

   Mfano: katika Kiingereza kipashio (-er) kikiunganishwa na baadhi ya vitenzi huleta maana ya mtu anayetekeleza(mtendaji) kitendo fulani ni mofimu moja. Mfano;

   run – runner

   sing – singer

   dance - dancer

Wakati mwingine kipashio hiki kinaleta maana tofauti, mf: broad - er, furth – er, clean – er ,cook-er,conner.

ii. Maumbo yenye maana moja lakini yanayotofautiana katika umbo la kifonetiki ambalo linaweza kuelezeka kifonolojia.

Maumbo haya huwa ni mofimu moja ijapokuwa yanatofautiana kifonetiki lakini kisemantiki yana maana moja. Mfano: Kipashio cha kinyume katika Kiingereza;

| | |
|---|---|
| {il} | illegal |
| {im} | impossible |
| {in} | incomplete |
| {un} | unnecessary |
| {ir} | irreversible |

Lakini huleta maana tofauti katika maneno haya: invaluable, incredible, indispensable

iii. Maumbo yenye maana sawa lakini yanayotofautiana katika umbo la kifonetiki huwa ni mofimu moja. Tofauti hizi za kionetiki haziwezi kuelezeka kwa urahisi kifonolojia na hazina utaratibu maalumu.Wingi katika Kiingireza kwa kawaida huwakilishwa na ‘s’ lakini matamshi yake hutofautiana katika mazingira mbalimbali.

Mfano: Kiingereza

| | |
|---|---|
| boy | boys (-iz) |
| pie | pies (s) |
| issue | issues (z) |

ox oxen (-en)

sheep sheep (φ)

Katika Kiswahili ngeli ya (ji-ma) sifa hii inajitokeza sura ya baadhi ya maneno inabadilika. Si rahisi kutambua majina ya ngeli hii.

mfano: ngeli ya (6) vambishi vina maana moja lakini maumbo tofauti ya kifonetiki.

(wingi: ma, me, na Φ; umoja ji, Φ).

| **Mofimu za umoja/wingi** | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|
| (ji) (me) | jiko | meko |
| Φ (ma) | karatasi | makaratasi |
| Φ Φ | jambazi | jambazi |

iv. Kutazama maumbile ya neno: Kama maneno yanayotofautiana kimaumbile tu huweza kuwa mofimu moja. Mfano: tooth-teeth.

v. Homofoni, hutambulika kuwa mofimu moja au mofimu tofauti kwa misingi ifuatayo. Hutamkika kwa njia sawa lakini yana maana tofauti.

meat –meet

pail – pale

flour – flower

sew – so

Homofoni zenye maana tofauti ni mofimu tofauti kabisa.

Homofoni zenye maana moja huwa ni mofimu moja.

vi. Kuangalia mofimu katika mikabala tofauti.

Mofimu inaweza kutambulikana kama;

a) Inaweza kujitenga mf, mofimu huru {paka}.

b) Inaambatanishwa kwenye kipashio kinachoweza kujitenga (mf: mofimu tegemezi).

{farm} + {-er}, {pig} + {an} + {a}.

c) Hujitokeza kama kiambishi pekee katika kitengo kinachoweza kujitegemea.

Mwanahewa – mwana + hewa

Askarijeshi – askari + jeshi

Mitishamba – miti + shamba

Alomofu.

Neno hili lina sehemu mbili ‘alo’ hili lina maana ya wingi,’mofu’ ni umbo halisi la mofimu.

Kwa hivyo ‘Alomofu’ni maumbo tofauti ya mofimu moja.

Sifa za alomofu;

a) Umbo halisi ambalo ni sehemu ya neno.

b) Ni mojawapo ya mofu za mofimu moja.

Alomofu ni sura tofauti za mofimu moja. Mfano wa alomofu za wakati ni /li/, /na/, /ta/, /po/, /ka/.Hizi ni alomofu za mofimu ya wakati.Pia alomofu za umoja katika ngeli ya kwanza ni; /m/, /mu/, na /mw/.Mfano;


mtu – watu

mwalimu – walimu

muumba – waumba

Katika mchoro ufuatao uhusiano wa mofimu,mofu na alomofu unaweza kuwakilishwa ifuatavyo;

Mofimu (ngeli 1)




Kauli ya kutendeka ina alomofu zifuatazo;

| | | |
|---|---|---|
| /ek/ | - | shoneka |
| /ik/ | - | pikika |
| /lek/ | - | toleka |
| /lik/ | - | valika |
| /ikan/ | - | takikana |
| /ekan/ | - | onekana |
| /likan/ | - | julikana |

Licha yakuwa na maumbo tofauti hizi ni alomofu za mofimu moja yaani jinsi ya kutendeka.

Jinsi ya kufanyiza pia ina alomofu kadha.

/I z/ fanyiza

/ez/ pendeza

/ish/ pigisha

/esh/ endesha

/liz/ tuliza

/lez/ koleza

/lish/ zalisha

Muhitasari.

Kufikia sasa tumeainisha dhana mbalimbali za mofolojia,ni vizuri kusoma vitabu vinavyozungumzia dhana hizi kwa undani.

**Aina za maneno ya Kiswahili.**

Wanasarufi wa mwanzo walianisha maneno ya Kiswahili katika makundi manane:

1. **Nomino/jina/nauni** ni neno linalotumiwa kutajia kitu; kitu kinaweza kuwa, mtu, mahali n.k.

   Mawasiliano hayawezi kukamilika bila nomino au kiwakilishi chake.

Wanaisimu wengi wanakubaliana Kiswahili kina aina zifuatazo za nomino;

a) Majina ya pekee(majina maalumu).

Haya ni majina yanayotaja vitu maalumu; watu, miji, nchi: Nairobi, Tanzania, Jumpili, Februari Otieno; majina haya yote haunza kwa herufi kubwa.

b) Majina ya kawaida.

Hutaja mtu au mambo yasiyo maalumu mf: kitu, gazeti, samaki, jembe.

Katika majina ya kawaida yamegawika mara tatu; wingi, dhahania(nomino za kufikirika) na jamii (nomino za makundi).

i. Majina ya dhahania.

Majina haya huwakilisha vitu ambavyo vinaweza kufikirika au kudhaniwa tu, visivyoweza kushikika au kuonekana, mfano: usingizi, uzalendo, upole, uvivu,werevu bidii n.k..

ii. Majina ya wingi.

Haya majina huwakilisha vitu vinavopatikana katika hali ya wingi tu: mf: maji, mafuta na mchanga,maziwa manukato,marashi, mate n.k.

Mfano katika sentensi; Mnyweshe mtoto mziwa.(Mziwa yawe mengi au yasiwe mengi yatarejelewa kama maziwa tu)

iii. Majina ya jamii(majina ya makundi)

Hutaja vitu ambavyo asili yake ni mkusanyiko lakini yanatajika kama kitu kimoja mf: timu, batalioni, baraza, kikosi, familia ,pakiti,jeshi n.k.

**2. Vivumishi.**

Haya ni maneno hutoa sifa zaidi za jina (yanayovumisha majina).

**Kuna aina mbalimbali za vivumishi;**

i. Vivumishi vya sifa.

Maneno yanayotaja tabia,yaani hueleza namna kitu kilivyo mf:

- dogo, -ema, -geni, safi, stadi,-kubwa,-eusi,-refu.

ii. Vivimishi vya idadi.

Huonyesha idadi ya vitu au mambo; mbili, chache, - ingi ,-ote

iii. Vivumishi vimilikishi.

Vivumishi hivi hujulisha mali ni  ya nani.

- angu, - ake, - ao – enu, na – etu.

iv. Vivumishi vionyeshi.

Huonyesha ujirani wa kitu na kingine au umbali wa kitu kwa uhusiano na kingine;

huu, hiki, hizi, hili, mle, kule, sile, pale.

v. Vivumishi viulizi.

- Pi, - ngapi, - ngapi, na gani.

vi. vivumishi vya pekee.

Huwa na upatanisho wa kipekee wa kisarufi.mfano;

- enye, - enywe, - ingine, ote na o-ote.

vii. vivumishi vya  a-unganifu.

mfano: Jeshi la mgambo

Mtu wa watu

Lugha ya wazee

Viatu vya shule

**3. Viwakilishi/pronomino/pronauni.**

Husimama badala ya majina.

Aina za viwakilishi;

i. Viwakilishi vionyeshi.

Huyu analala.

Ule haupenda.

Huku hakukaliki.

Humo humkaliki.

iii. Viwakilishi viulizi.

Mfano;-pi, gani, ngapi

Yupi unayemtaka? (kuku)

Ngapi zimeshonwa? (nguo)

Wangapi wamebaki? (kondoo)

iii. Viwakilishi vimilikishi

mfano: - angu, -etu, -ake, na –ao

pako pachafu.

**4. Vitenzi.**

Haya ni maneno ambayo hueleza kufanyika kwa jambo.

**Kuna aina mbalimbali za vitenzi.**

i. Vitenzi vikuu: Hutaja matukio mbalimbali mf: Maria anaandika.Kitenzi kikuu ni anaandika.

ii. Vitenzi vishirikishi.

- Hushirikisha/ kulete uhusiano baina ya; jina, kwakilishi, kivumishi au kielezi na jina, mf: Baba ni mwenyekiti wa kijiji.

  Amina alikuwa mwalimu.

iii. Vitenzi visaidizi.

- Hutimika sambamba na vitenzi vikuu katika sentensi ili kukamilisha maana

  Mfano: Juma angali analima.

  Wanajeshi walikuwa wanapanda mlima.

**5. Vielezi.**

Neno/maneno yanayoelezea kuhusu tendo linalofanyika.

Kuna aina nyingi za vielezi;mahali,wakati,idadina na mna(jinsi)

i) Vielezi vya mahali.

   Hueleza zaidi matendo kuhusu mahali yanapofanyika.

   Mf: Anapanda juu.

   Ameenda Nairobi.

ii) Vielezi vya wakati.

- Hufafanua wakati matendo yanapotokea.

Mfano: Alifika jana.

Mtihani utaanza saa tatu.

iii) Vielezi vya idadi .

Hutujulisha tendo limetokea mara ngapi.

Mfano: Nimekuja mara tatu.

Yeye hufika shuleni mara chache.

iv) Vielezi vya namna/jisni.

Hueleza jinsi(namna) tendo linavyofanyika

Mf: Anatembea polepole.

Alilala fofofo.

Alivaa kizungu.

**6. Viunganishi.**

Viunganishi huunganisha neno kwa neno, neno kwa kikundi au sentensi kwa sentensi

Mf: mtoto hakulia wala kuleta matata.

Viunganishi: lakini, au, ila, kwa sababu, hata kama ilhali, halafu, kwa kuwa.

**7. Vihisishi.**

- Hudokezea hisia, mguso, au vionja vya ndani vya mzungumzaji.

- Maneno haya hudhihirisha kebeli, uchungu, furaha, shangwe, mshangao au utambuzi

  Mfano: Ala!, ebo!, kumbe!

8. **Kihusishi.**

   Huonyesha uhusiano uliopo baina ya maneno, fungu la maneno au sentensi mf: wa, ya, cha, kwa, na za.

Mfano: Nguo za Juma zimepotea.

Alisafiri kwa gari.

**Kuna udhaifu unaotokana na kuyatenga maneno katika aina nane.**

Uainishaji wa aina za maneno kwa kutumia nadharia(mwongozo) ya sarufi mapokea una upungufu mkubwa.

i. Baadhi ya maneno hupatikana katika makundi tofauti: mf: vivumishi hutumika kama vielezi au nomino.

   Mfano: Vitabu vizuri (kivumishi)

   Anatembea vizuri (kielezi)

   Uzuri ni utu (nomino)

Ni vigumu kuainisha neno zuri kwa njia hii. Pendekezo ni kuwa maneno yangeainishwa kutegemea uutendakazi wake katika sentensi.

ii. Maelezo na maana ya aina hizi za maneno si dhahiri; hayatokani na utafiti wowote, hayaeleweki, hayatenganishwi. Mtu analazimika

kuwa analijua neno kutoka awali ili kujua ni neno la aina gani linalozungumziwa.

iii. Maelezo kuwa kiwakilishi ni neno litumiwalo badala ya nomino,hayaelezi kuwa neno lolote lile linaweza kutumika badala ya nomino.

iv. Lugha zingine huenda zikawa na zaidi ya aina nane za maneno. Vielezi huwa na maneno ambayo hayahusiani.

Mfano: Haraka sana.

1. Alikimbia sana. (kielezi 1)

2. Alikimbia haraka sana. (kielezi 2)

3. Mtoto mzuri sana. (kivumishi).

Maneno kama sana, mno, kabisa yana utendakazi maradufu licha yakuwa vielezi.

**Licha ya udhaifu huu nadharia ya wanaisimu wa jadi ina umuhimu kwa kuwa;**

i. Walichochea watafiti wengine kutoka sehemu zingine za ulimwengu kutafiti lugha kisayansi; na kuanzishwa kwa nadharia zingine za sarufi.

ii. Walianzisha istilahi na dhana nyingi zinazotumika katika isimu ya leo mf: nomino, viwakilishi,vitenzi, sentensi, vishazi.

iii. Istilahi za wanamapokeo zilianza kupanuliwa na kutumika katika lugha nyingi za ulimwengu.

iv. Wayunani ndio walikuwa watu wa kwanza kutumia kategoria za kisarufi zinazotumiwa leo kama jinsia, unyambulishaji, idadi, wakati na hali.

Wanamapokeo walitumia njia mbili kuu katika kupanga ngeli za nomino kwa;

i. Kutumia viambishi,Viambishi awali vya nomino katika umoja na wingi vilitumika kama vitambulisho vya ngeli. Viambishi vya nomino vilitumika na wala si aina nyingine yoyote ya viambishi.

   Waliotumia mtindo huu ni kama vile: Krapf (1882), Burt (1917)

   Broomfied (1961) na Ashton (1944).

ii. Pia wanamapokeo walitumia isebati /nambari, 1, 2,3 hadi 18 kuainishia ngeli za nomino.Mfano wa waliotumia mtindo huu ni, Bleek (1869), Polome (1967) Myachina (1981).

**Ngeli za nomino kwa kutumia isebati na viambishi vya nomino.**

Nomino katika hali ya umoja ilichukuliwa ngeli moja na ikiwekwa katika hali ya wingi ilichukuliwa kuwa ngeli nyingine tofauti mfano;nomino;mtu iko ngeli ya kwanza na watu ngeli ya pili.

Kwa jumla viambishi vya ngeli ni M-WA, M – MI, JI-MA, KI-VI, N-N, U. na viambishi vya mahali PA, KU, MU.

Kwa kutumia isebati ngeli zilizoainishwa ni, 1,2,3,4,5,6,7,8,9,10,11,(12,13) 14, 15,16,17 na 18 ngeli za (12,13) hazipo katika Kiswahili sanifu lakini zinapatikana katika baadhi ya lugha za kibantu kulete maana ya undogo yaani ngeli ya KA/TU

Katika kuainisha ngeli kwa kutumia njia ya kimapokeo (kijadi) miundo yote miwili (nambari na viambishi hutumika pamoja).

| Nambari | Viambishi | Mifano |
|---|---|---|
| 1 | M | mtu |
| 2 | WA | watu |
| 3 | M | mkono |
| 4 | MI | mikono |
| 5 | JI | jibwa/jani |
| 6 | MA | majibwa/majani |
| 7 | KI | kijiti |
| 8 | VI | vijiti |
| 9 | N | nyumba |
| 10 | N | nyumba |
| 11/14 | U-(N) | uta /nyuta |
| (12) | (KA) | kamtu |
| (13) | (TU) | tumtu |
| 15/17 | KU | mahali kule/kucheza |
| 16 | PA | mahali pale |
| 18 | MU | mahali mle |

Nonino za ngeli ya 11/14 hutumia kiambishi U katika umoja.Nomino za ngeli ya 11 huanzia na –N katika wingi. Nomino za 11 zina wingi na zile za 14 hazina.

Nomino za ngeli ya 15/17 hutumia kiambishi KU.Nazo nomino za ngeli ya 15 huundwa kutokana na vitenzi. Ngeli ya 17 huwa ni nomino ya mahali pasipo maalumu.

Ngeli ya 12 na 13 hazipo katika Kiswahili sanifu lakini hupatikana katika lugha nyingi za kibantu-huitwa ngeli ya KA/TU

Wanamapokeo pia walitumia kigezo cha kisemantiki katika kuianisha nomino katika makundi maalumu.Hili ni jaribio la kuweka pamoja nomino zinazoleta maana moja.

Kigezo cha kisemantiki (maana)

| Ngeli | Maana na mifano ya nomino. |
|---|---|
| M –WA | Viumbe vyenye uhai. Majina ya binadamu n.k. |
| M – MI | Vitu visivyokuwa na uhai. Sehemu za mwili, vifaa, miti. |
| JI – MA | Sehemu za miti, vifaa, vya, kazi, ukubwa, vitu visivyohesabika, matunda. |
| KI – VI | Vifaa, baadhi ya wanyama, udogo. |
| N – N | Ngeli hii ndiyo kubwa zaidi. Vifaa, matunda, wanyama wadudu, watu majina ya mikopo. |
| U – N | Sehemu za mwili, hali zinazodhihirika na za kidhahania, Vitu visivyohesabika, nchi. |
| KU | Nomino zinazotokana na vitenzi. |
| PA, KU, MU | Mahali;maalumu,kusikodhihirika na ndani. |

Kuna matatizo mengi yaliyotokana na uinisho wa ngeli kwa kutumia mpangilio wa kisemantiki na kimofolojia (mtindo wa kijadi) pia kuna marekebisho yaliyopendekezwa.

**Matatizo**

Mpangilio wa ngeli kwa kutumia viambishi na isebati ulilenga kutumia misingi ya kimofolojia na kisemantiki.

Mipangilio hii haikuridhisha kutokana na matatizo mengi yalyoikukumba;

i. Mpangilio wa kimofolojia na kisemantiki unatenga maswala ya kisintaksi (mpangilio wa maneno katika sentensi) – ambayo ndiyo muhimu katika sarufi ya lugha yoyote.Kuna baadhi ya watalaamu ambao husema mtoto hujifunza lugha kwa kusikiliza sikiliza sentensi zinazotungwa na watu wakubwa.

ii. Hakuna makubaliano ya idadi ya ngeli za nomino miongoni mwa wataalamu mbalimbali;Kapinga (1983),anasema ni 9 lakini zikapanuliwa na kufika 14 ,Mohammed (2002), anasema ni 7 na Mgullu (1999), katika uchanganuzi anapata 12.

iii. Kutapakaa kwa majina katika zaidi ya ngeli moja.

Mfano:

a) Majina ya binadamu.

5/6 JI/MA – dereva/madereva.

7/8 KI/VI – kiwete/viwete.

9/10 N/N – seremala/seremala.

c) Sehemu za mwili.

7/8 -Kidole/vidole.

5/6 JI/MA – jicho/macho.

7/8 KI/VI – kichwa/vichwa.

9/10 N/N – nywele /nywele.

11/14 U/N – wayo/nyayo.

c) Vifaa .

3/4M/MI – mshipi/mishipi

5/6 JI/MA – jiko/meko

7/8 KI/VI – kisu/visu

9/10 N/N – meza/ meza

11/14 U(N) – uteo/teo

d) Wanyama.

½ M/WA – mnyama/mishipi

5/6 JI/MA – Jibu/majitu

7/8 KI/VI – chura/vyura, kifaru/vifaru

9/10 N/N – ng’ombe –ng’ombe

Matumizi ya viambishi sawa katika ngeli, mbalimbali.

M- majina ya 1/3

U – majina ya 11/14

KU – majina ya 15/17 ambayo hayana uhusiano wowote. 15 – kitenzi – jina na 17 mahali.

Majina mengi hayachukui viambishi vya makundi yaliyowekwa.

5/6 JI/MA – hayachukui JI katika umoja.

9 (N-) na (11-U-) hayachukui viambishi hivyo. (9N-) mf: samaki, kuku, taa n.k.

iv) Nomino za kukopwa hazina viambishi sawa na vigumu kujua zitawekwa kwenye ngeli gani mfano;baiskeli,motokaa n.k.

v) Uainishaji wa nomino kijozi, maneno mengine hayapatikani katika jozi. Mfano; Kikamba, Kijaluo, Kiswahili, hayana wingi nomino zingine zinapatikana katika hali ya wingi tu mfano: maji, mafuta,maziwa,mate n.k.

vi) Majina yasiyo na wingi wala umoja yamelundikwa katika ngeli ya 9/10 na hayahusiani kisemantiki.Mfano;chai,samaki,gari n.k.

vii) Ngeli ya 12/13 tayari zimetoweka kutoka lugha ya Kiswahili na hakuna sababu ya kuzidumisha kunaendeleaza ‘sheng’.

**Ngeli za nomino kwa kufuata upatanisho wa kisarufi**.

Kutokana na matatizo haya wanaisimu wamependekeza marekebisho**.**Mpangilio wa kisintaksia ulipendekezwa katika uainishaji wa ngeli za nomino, ulizingatia upatanisho wa kisarufi kwa kurejelea viabishi awali vya vitenzi, vivuvumishi, viwakilishi, vielezi, viunganishi na virejeshi. Jumla ya makundi kumi na moja yalianishwa kw kufuata upatanisho wa kisarufi.

a) Ngeli ya A-WA.

Nomino zote zinazochukua kiambishi A katika umoja na WA katika wingi, katika upatanisho wake wa kisarufi na kiambishi awali cha kitenzi katika sentensi

Mfano: Mtoto analia. Watoto wanalia.(a-wa)

Mbuzi ameuzwa. Mbuzi wameuzwa.(a-wa)

Ngeli hii ya A-WA hujumuisha majina ya vitu vyenye uhai; watu wanyama, ndege, wadudu, na majina ya watu wanaofanya kazi mbalimbali.Mfano;mlinzi-walinzi.,mkulima –wakulima.

b) Ngeli ya U-I.

Nomino huchukua ukubaliano wa U katika umoja na I katika wingi zikitumiwa na vitenzi.

Mfano: Mkeka umekauka. Mikeka imekauka.(u-i). Mchungwa umekatwa.Michungwa imekatwa.

c) Ngeli ya U-YA.

Nomino huchukua kiambishi U katika umoja na YA katika wingi katika upatanisho wake wa kisarufi na kiambishi awali cha kitenzi katika sentensi.

Mfano: Ugonjwa umezidi. Magonjwa yamezidi.(u-ya)

Hujumuisha matokeo ya vitu ambavyo havionekani.Hata hivyo athari ya vitu hivyo hudhihirika.

d) Ngeli ya YA-YA.

Majina ya vitu ambavyo mara nyingi huwa katika hali ya wingi. Huchukua upatanisho wa YA-kwa umoja na wingi.

Mfano: Maji yamekwisha. Mmaji yamekwisha.(ya-ya)

e) Ngeli ya LI-YA.

Nomino huchukua kiambishi LI katika umoja na YA katika wingi, katika upatanisho wake wa kisarufi na kiambishi awali cha kitenzi katika sentensi.

Mfano: Jicho linauma . Macho yanauma.(li-ya)

f) Ngeli ya KI-VI

Huchukua KI katika umoja na VI katika wingi yakiambatanishwa na vitennzi katika sentensi.

Nomino zingine huchukua CH-katika umoja na VY –katika wingi.

Mfano: Kisu kikuwa kimepotea – Visu vikubwa vimepotea.(ki-vi)

Choo kimeoshwa-Vyoo vimeoshwa.( ch -_vy- )

g) Ngeli ya I-ZI.

Nomino zinazochukua kiambishi I katika umoja na ZI katika wingi katika upatanisho wa kitenzi katika sentensi.

Mfano: Nguo imekauka – Nguo zimekauka.(i-zi)

**h) Ngeli ya I-I.**

Ngeli hii hujumuisha majina ya vitu visivyohesabika kimoja kimoja ila kutokana na vipimo maalumu. Majina katika ngeli hii huchukua viambishi I-I kwa umoja na wingi katika upatanishi wa kisarufi yakitumiwa pamoja na vitenzi katika sentensi.

Mfano: Asali imenwagika – Asali imemwagika.(i_i)

**i) Ngeli ya U-ZI.**

Nomino hizi huchukua viambishi U kwa umoja na ZI katika wingi zikitumiwa na maneno mengine ya lugha kuonyesha ukubaliano wa maneno na upatanisho wa kisarufi.

Mfano: Ukope umerefuka – Kope zimerefuka.(u-zi)

Nomino zingine huchukua ukubaliano wa viambishi hivi lakini kwa wingi huanzia kwa NY – mf: unyasi –nyasi ,uta – nyuta, uso –nyuso, ua –nyua.

Mengine huanza kwa W-mfano; waya – nyaya.

**j) Ngeli ya U-U.**

Nomino huchukua kiambishi U kwa umoja na U katika wingi zikitumiwa na vitenzi na maneno mengine ya lugha kuonyesha ukubaliano wa kisarufi katika sentensi.

Mfano: Ugali umeiva, Ugali umeiva., Uchungu umezidi –Uchungu umezidi.

**k) Ngeli ya KU.**

Nomino huundwa kutokana na vitenzi. Vitenzi huongezewa kiambishi –ku mfano;lima-kulima

Nomino katika ngeli hii huchukua kiambishi KU katika upatanisho wa kisarufi baina ya vitenzi na nomino zenyewe.

Mfano: Kucheza kwake kulivutia.

Kulia kwenu kunanihusunisha.

**l) Ngeli ya PA/KU/MU.**

Hii ni nomino moja ambayo ni neno mahali na ambayo huchukua viambishi hivi vitatu kutegemea ukubaliano wa kisarufi na maneno mengine katika sentensi kudhirisha mahali aina tatu maalumu, karibu (maalumu), ambapo si maalumu (kusikodhihirika), na ndani.

Mfano; Mahali hapa ni pachafu.

Mahali huku kumepambwa.

Mahali mle mnatisha.

**Dhana ya viambishi.**

Dhana ya viambishi inaweza kufafanuliwa kwa kusema; ni silabi zinazofungiliwa kwenye mzizi wa kitenzi ili kuleta maana mbalimbali.(Silabi zenye maana zinawezakuwa mofimu).

Muundo wa kitenzi cha lugha ya Kiswahili, huwa na viambishi mbalimbali.

a) Viambishi awali.
b) Mzizi wa kitenzi.
c) Viambishi tamati.

Mfano: Kanushi + njeo + mzizi + tamati

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Sitacheka | {si} | + | {ta} | + | {lim} | + | {a} |
| Viambishi- | (awali)+ | | (awali) | + | mizizi | + | tamati |

a) Viambishi awali hutokea kabla ya mizizi wa kitenzi na vinaweza kuleta maana mbalimbali.

i. Kanushi – sikulala

ii. Njeo – Juma alienda.(-li-)

iii. Hali mbalimbali anaimba, ameimba, huimba.(-na-)

iv. Vipatanishi – Nguo imepasuka.(-me-)

v. Masharti: (nga), (nge) (ngali), (ngeli).

vi. Rejeshi: Namna anavyoimba, atashinda.(-vyo-)

vii. Yambwa: seremala aliukata mti.(-u-)

viii. Kujitendea: nilijikata.(-jio-)

b) Mzizi wa kitenzi

Ile sehemu ya kitenzi ambayo haibadiliki baada ya viambishi mbalimbali kuongezewa au kuondolewa.

Mfano: -/a/-, -/a/-, -/I/-, -/F/-, -/pig/-, -/lim/-, -/chez/-,

c) Viambishi tamati (mwisho).

Viambishi tamati huongezwa baada ya mzizi wa kitenzi .

i. Vimalizio mfano: lim – a, haimb-i.(-a na –i ni vimbishi tamati)

ii. Alomofu za jinsi mbalimbali mfano: pend-e-zwa, za-li-shwa, pig – ik –a.

iii. Viambishi elezi mfano: alifikaje, Napenda anndikavyo.(-je,-vyo).

## SURA YA TATU.

### Uundaji wa maneno.

### Sababu za uundaji wa maneno mapya.

Somo la mofolojia huhusisha uundaji wa maneno mapya. Lugha zote duniani hukua ili ziweze kurejelea dhana mpya zinazotokana na maendeleo katika maisha ya binadamu.Kuna sababu nyingi zinazochangia uundaji wa istilahi na msamiati mpya katika lugha;

i) Kuelezea dhana mpya zinazobuniwa au kuibuka.

ii) Maendeleo katika nyanja mbalimbali za maarifa ya binadamu, sayansi, uchumi, teknolojia na sheria.

iii) Uchakavu wa maneno ya awali mfano;damu -zamani iliitwa ngeu.

iv) Sababu za mila;Jamii hujiepusha na matumizi ya baadhi ya maneno ambayo ni ni mwiko kuyatja wazi wazi.Mfano; badala ya kusema kuzaa- tunasemakujifungua.

v) Maingiliano ya kijamii, huleta haja ya msamiati mpya kuelezea muingiliano huo.

vi) Kufanikisha mawasiliano baina ya taasisi, matabaka na mashirika mbalimbali.

### Mbinu za kuunda msamiati na istilahi.

a) Mwambatano.

Kuunganishwa kwa maneno mawili kuzua, neno moja lenye maana mpya (tofauti) na maneno yaliyoliunda:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| N | +N | mwana + | jeshi - | | mwanajeshi |
| | | Mbata + | mzinga- | | mbatamzinga |
| N | +Kt | mwamba + | dukiza- | | mwambadukiza |
| N | +Kv | ng’ombe + | jike - | | ng’ombejike |
| | | Mja + | mzito - | | mjamzito |
| Kt | +N | Pima + | mvua - | | kipimamvua |
| | | Changa + | moto - | | changamoto |
| | | Saga + | gego - | | sagagego |

Upungufu wa mbinu hii ni kuleta uzito wa kisemantiki kutokana na maana ya awali ya maneno. Yafaa yatumike mpaka yazoeleke.

b) Unyambuaji

Viambishi huongezwa kwanya mzizi kuzua neno jipya.

i. Unyambuaji kwa kutumia viambishi hupanua maana ya neno mf:

Mzizi: piga

- kupiga
- pigo
- pigana
- mapigano

ii. Unyambuzi kutokana na mizizi mingine

| Mzizi | Neno lililoundwa |
|---|---|
| zuri | uzuri |
| jamaa | ujamaa |

iii. Unyambuaji wa viambishi ili kuunda nomino.

| Kitenzi | Nomino |
|---|---|
| tafiti | utafiti |
| chuma | uchumi |

c) Kukopa

Mbinu inayotumiwa na lugha zote kurutubisha msamiati wake.

Sababu za kukopa

i. Neno lililokopwa husimamia kitu ambacho hakipo kitaka utamaduni kopaji.
ii. Kasumba ya kupendelea mambo fulani kuliko mengine:mf:

| | | |
|---|---|---|
| kuanguka- | | kufeli |
| kupita | - | kupasi |
| pinde | - | kona. |

iii. Maingiliano marefu ya kitamaduni na kijamii.
iv. Utabaka, lugha ya tabaka la china hukopa kutoka kwa tabaka la juu.

Kiswahili kimekopa kutoka lugha za kiafrika na za kigeni. Maneno yale ya kigeni hupewa muundo wa KVKV (kosonanti vokali) ambao ndio muundo asili wa lugha ya Kiswahili.

Mfano:

| Lugha kopeshaji | Mfano wa maneno |
|---|---|
| Kihindi | pesa, bima, laki, godoro |
| Kituruki | baruti, bahasha, korokoro |
| Kireno | karata, bendera, mvinyo |
| Kijerumani | hela, shule |
| Kiingereza | Mei, daktari, kampuni, eropleni |
| Kiarabu | rehema, faraja, alhamisi. |

**Njia za ukopaji.**

1) **Kukopa kwa tafsiri.**

Kifungu katika lugha asilia hutafisiriwa katika lugha kopaji. mfano:

Electoral Commission-Tume ya Uchaguzi.

Opposition party-chama cha upinzani.

Commissioner general- kamishena mkuu.

Upungufu wa mbinu hii ni kuwa wawezapata tafriri ambazo hazileti maana inayokusudiwa mf.

Mobile phone- simu za kurandaranda (simu za mikono)

Sick leave- likizo ya ugonjwa

Dictatorship- uongozi wa imla (uongozi wa kimabavu)

2) **Utohozi**

Neno kutoka lugha asilia hunukuliwa kwa kufuata fonolojia ya lugha pokezi. Maneno yaliyotoholewa hupata maana kutoka kwa lugha pokezi. mf.

atom- atomi office- ofisi

virus- virusi doctor- daktari

Upungufu wa mbinu kutofuata utaratibu maalumu;

Mfano: dance- dansi/densi officer- afisa/ ofisa

bank- banki/benki

Utohozi; utilie maanani lugha pokezi

Kukopa sisisi (ukopaji wa moja kwa moja).

Neno huchukuliwa lilivyo katika lugha changizi na kutumiwa katika lugha kopaji.

Mfano:

| **Neno** | **Lugha changizi** |
|---|---|
| Kitivo | kipare |
| ikulu | kinyamwezi |
| kasri | kihindi |
| mbunge | kisukuma |

**Ufupishaji.**

Mbinu za ufupishaji.

i) Ufupishaji mkato.

Vifungu vichache hutumika.

| **Kiingereza** | **Kifupisho** |
|---|---|
| Jumbojet | jumbo |
| examination | exam |
| memorandum | memo |
| photograph | photo |
| **Kiswahili** | **Kifupishio** |
| Bibi | Bi. |
| Baba | Ba. |

ii) Akironimu.

Kutumia silabi za mwanzo za maneno fulani katika kirai kuunda neno: mf, ukosefu wa kinga mwilini: ukimwi. Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili TUKI. Chama cha Kiswahili cha Taifa. CHAKITA.

iii) Uhulutishaji

- Virai hufupishwa ili kupata maneno.

  Sehemu ya mwanzo ya kirai cha kwanza huunganishwa na sehemu ya kwaza ya neno la pili kuunda neno jipya. Mfano;

  - Msikwao- mtu _ asiye+ kwao
  - Chajio- chakula_ jioni
  - Mala- maziwa +lala

  Udhaifu wa mbinu hii: visemu ambavyo si vya mwanzo hutumika pia: mfano.

  - huhaba- huduma hadi bandarini.
  - runinga- rununu+maninga.

  Wakati mwingine shina nzima hutumika mf.

  - kiua+dudu- kiuadudu
  - Ute+mayai- uteyai (egg york)

  Ukosefu wa mantiki wa kutekeleza mbinu hii kwa ujumla. Hasa kwa kuamua ni kirai kipi kitakachotumika; mf. Fupaja kutoka kwa mfupa wa paja-je kwa nini si mfupaja?

**Kubuni.**

Kuna njia mbalimblai za kubuni msamiati.

i) Kubuni kwa kinasibu;

Mbinu hii huzifanya fonimu za lugha kulingana na utaratibu wa ujenzi wa lugha.

Kubuni maneno mapya hupuguzia maneno yaliyopo katika lugha mzigo wa kubeba maana zaidi. Mfano;

- Ndge- kisopo
- Golo- bureau de change

Njia hii ina upungufu, neno linalobuniwa laweza kutokuwa na uhusiano na dhana linayosimamia/kitu kinachotajwa. Huwa kuna tatizo kama watumiaji hawakuhusishwa katika uundaji wake.Waliolengwa huenda walikatae neno.

ii) Kubuni kwa kuongozwa na vigezo maalumu, mfano: maumbile, tabia na matumizi

Ubunifu huu hufuata misingi ya kionamatopea kupata majina. Mfano.

- pikipiki
- tingatinga
- gari la moshi
- kifauawongo
- mtandao

Upungufu- inamfunga mwundaji wa istilahi kuambatanisha neno na kitajwa; jambo ambalo haliwezekani wakati wote.

**Uwawilishaji/uhamishaji**

Kuhamisha vipashio vya neno kuchukua nafasi tofauti katika neno jipya linaloundwa.

Pia maana ya awali huhamishwa na neno hupata maana mpya. Mf:

- vyaa (kuzaa) - avya (kuhamisha sauti)
- kupe (mnyama) - mtu anayetegemea
- kifaru (mnyama) - gari la kivita.

a) Kurudiarudia

Kurudia neno au sehemu ya neno ili kuleta maana mpya. Mfano:

- Kizunguzungu
- Pikipiki
- Polepole

b) Ugeuzaji

Neno linageuzwa kutoka kikundi kimoja kisarufi na kuingizwa katika kikundi kingine, mfano: Cheza –[kitenzi]- mchezaji [nomino].

Okoa- mwakozi/wokovu

**Matatizo katika uundaji wa maneno.**

i) Maneno kubeba uzito kimaana(uzito wa kuyatumia maneno); inabidi neno litumike mara nyingi ili lizoeleke.

ii) Kuwepo kwa istilahi/maneno mbalimbali kwa neno moja mf.

- nomino- jina/nauni

- runinga-televisheni
- mavi; kinyesi, mlima, kimba

iii) Kutokuwa na utaratibu maalumu (ukosefu wa ruwaza moja) mf katika Somo la;

(a) Baolojia;

- Plasmagene- utoroji
- Plasmalima-ugoziuwili
- Plasmadesta- kiuzichembe

(b) Katika isimu:

base-msingi/kiini cha neno

baseform- umbo msingi

basecompund- neno ambatano, neno msingi lapotea katika maana ya tatu.

iv) Kutopata "ukubalifu wa kimataifa"

| **Neno** | **Neno lililopendekezwa** | **Neno ambalo lina umataifa** |
|---|---|---|
| mirage<br>hydrophite<br>hydrotropism | mazigazi<br>yugiyugi<br>ubadilihali | Miraji<br>hydrofite<br>hydrotrophisimu |

v) Kuwepo kwa istilahi nyingi kwa dhana moja – (kutosanifishwa) mf:

Sauti:/ m,n,ng' n any/ huitwa sauti za nazali, nasali, vingongo'o au vipua.

vi) Dhana zilizotoholewa hasa katika lugha za kiafrika ni gumu kutafsiri kama mtu hajui lugha asilia.

g) Katika kutafsiri wakati mwingine maana ya kimsingi hupotea (dhana ya msingi iliyokuwa katika istilahi za lugha chasili). Mfano:

| **Lugha msingi** | **Tafsiri** |
|---|---|
| National Bureau of Standards | Ofisi ya vipimo vya taifa |
| Reception | mapokeoni |
| | |

**Maswali.**

1. Fafanua mofolojia ya nomino ya Kiswahili ukitumia vigezo vifuatavyo;

    (a) idadi.

    (b) ukubwa na undogo.

    (c) udhalilishaji.

2. Ukitoa mifano fafanua kikamilifu unominishaji katika Kiswahili.

3. Jadili muundo wa kitenzi cha Kiswahili ukizingatia yafuatayo;

    (a) umbo.

    (b) viambishi awali, kati na viishio

    (d) Majukumu ya kisarufi na kileksia ya viambishi hivi.

4. Eleza mofolojia ya kategoria zifuatazo za maneno katika Kiswahili;

(a) vivumishi.

(b) viwakilishi.

(c) vielezi.

(d) vihusishi.

5. Taja na eleza kauli mbalimbali za kitenzi cha Kiswahili.

**Marejeleo.**

Habwe ,J na Karanja,P. 2007: Misingi ya Sarufi ya Kiswahili:Nairobi,Phoenix Publishers.

Mgullu,R.1999:Mtaala wa Isimu. Nairobi:Longhorn Publishers.

Nkwera ,F.M :1978:Sarufi na Fasihi; Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam.Tazania Publishing House.

## SURA YA NNE.

### Sintaksia ya Kiswahili

**Sintaksia**: Kiwango cha isimu ambacho hujishughulisha na uchanganuzi wa mpangilio wa maneno katika sentensi na hujishughulisha na vipashio vyake.

Kwa mujibu Habwe na Karanja(2004), sintaksia ni utanzu wa isimu unaoshughulikia muundo wa sentensi na elementi nyinine znazounda sentensi kama vile kategoria za maneno,vikundi na vishazi.

Kuna sheria ambazo hazina budi kufuatwa katika kuyapanga maneno ya lugha katika mfuatano (neno moja baada ya lingine)- kwa namna ambayo maneno hayo yatalete maana inayokubalika na kueleweka katika lugha husika.

Sintaksia ya lugha- hufafanua sheria zinazoongoza mpangilio wa maneno katika sentensi katika lugha hiyo, ili kuonyesha maneno ambayo ni lazima yatangulie au yafuate mengine.

Sintaksia pia huzingatia uhusiano wa maneno katika tungo na kueleza maneno yanayomiliki mengine katiaka sentensi.

Sintaksia pia hueleza aina mbalimbali za sentensi katika lugha.

Uchanganuzi utakaofuata utaongozwa na sarufi miundo virai na sarufi geuza umbo.

### Sarufi miundo virai

Sarufi miundo virai ni kitengo cha sarufi geuza umbo hujihusisha tu na viambajengo (vipashio vya sentensi).

Kanuni miundo virai hutumiwa katika kuonyesha na kueleza viambajengo vya sentensi. Kanuni hizi  huonyesha maana ya sentensi.

Kanuni hizi ndizo huunda sarufi virai. Kwa kutumai kanuni hizi sarufi hii inaweza kuzalisha sentensi nyingi.

Kupitia kanuni hizi vijisehemu tofauti vya tungo vinaweza kupewa majina na pia kuelezwa kisarufi. Jambo hili halingewezekana kupitia upambanuzi wa viambajengo.

Sheria za sarufi miundo virai huandika upya sehemu zote za tungo hadi kufikia kiwango cha mofimu.

Jinsi ya kueleza kanuni hizi.
Mfano wa sentensi;
Mti mrefu umeangukia nyumba nzuri.

Sentensi hi inawezakuzalishwa kupitia kanuni sita.

i) S - KN + KT

ii) KN - N + KV

iii) KT - KT + KN

iv) N - m-ti, nyumba

v) KV - mrefu, - n-zuri

vi) Kt - uli-anguk-i-a

Tunaweza kutumia kanuni hizi na kuunda sentensi nyingine kwa kutumia maneno yale yale lakini katika nafasi tofauti (ni muhimu kutilia maanani upatanisho wa kisarufi) mfano;

Nyumba nzuri iliangukia mti  mrefu.

Nyumba ndefu iliangukia mti mzuri.

Mti mzuri uliangukia nyumba ndefu.

**Vipashio vya sentensi.**

Sentensi ndicho kipashio kikubwa cha kisarufi katika lugha kikiwa kimeundwa kwa vipashio vidogo vidogo kama vile: neno, kirai au kikundi (kifungu /kishazi).

i. Neno.

Mdee (1986) neno ni fungu la silabi ambalo lina mkaazo mmoja. Vipashio vya neno ni maneno yoyote yenye maana ambayo yanatokana na aina za maneno. Mfano:

- Jina/nomino- mtoto, Juma, Kisumu
- Kivumishi- baya, -zuri, -eupe
- Kitenzi- cheza, lala, imba
- Kielezi- sana, polepole, tatu, uskiu
- Kiwakilishi- yeye, wewe, ni-
- Kihisihi- lo!, hewala! Kumbe!
- Kiunganishi- lakini, na, kwa, ilhali
- Kihisishi- chini ya, kando ya, na

ii. Kirai (kifungu/kikundi).

Kipashio cha kimuundo chenye zaidi ya neno moja lakini hakina muundo wa kiima- kiarifu. (muundo huu huhusisha mtendaji wa kitendo na kitendo kinachotendwa).

Mundo wa kiima- kiarifu- ni wa kimsingi katika sentensi za lugha yoyote ile.

Kirai huundwa kutokana na mahusiano maalumu baina ya maneno. Mahusiano haya yanadhihirisha kwamba uundaji wa virai umekitwa katika aina za maneno. Virai vitaainishwa kwa mujibu wa aina za maneno.

**Aina za virai.**

- Kirai – nomino (KN)
- Kirai – kivumishi (KKV)
- Kirai – kitenzi (KT)
- Kirai – kielezi (KKL)
- Kirai-kiunganishi (KKU)
- Kirai – kiwakilishi (KKW)
- Kirai- kihushi (KKH)
- Kirai - kihisishi(KKI)

**Kirai – nomino**

Muundo wake umekitwa kwenye nomino au mahusiano ya nomino na neno a mafungu ya maneno. Mfano:

a) Nomino peke yake KN → N

   Swala anawindwa.

b) Nomino mbili na zaidi KN → N+N

   Shangazi na mgeni wameingia.

c) Nomino na kivumishi KN → N+KV

   Mbuzi mnono amechinjwa.

d) Nomino na sentensi KN → N+S


   Mtoto aliyemletea mama yake kuni jana ametoroka.

e) Nomino, kivumishi /vivumishi na sentensi KN → N+ KV +S


Mwalimu mrefu anayefundisha sayansi katika shule ya upili ya Nairobi amehamishwa.

**Upanuzi wa tungo .**

Mkulima amevuna**.**




Shangazi na mgeni wameingia




**Kirai kitenzi**

Kirai hiki kimekitwa katika kitenzi au katika mahusiano ya kitenzi na neno au mafungu mengine ya maneno. Neno kuu katika aina hii ya virai ni kitenzi. Mchanganuzi huzingatia kitenzi na maneno yanayokifuata katika sentensi.

**Miundo ya kirai-kitenzi**

a) Kitenzi pekee KT $\rightarrow$ Kt

Asha amekula

b) Kitenzi na nomino KT → Kt +N

Watu wamekata mti

c) Kitenzi na nomino kitenzi KT → Kt + N + Kt

Tumemlazimisha Juma kula.

d) Kitenzi (na kiramba/kuwa na sentensi)

KT → Kt + (sentensi yenye kuwa)

Mwalimu amesema kwamba atarudi kesho.

**Kirai kivumishi**

Hujikita kwenye kivumishi katika muundo wake.

Aina za virai vivumishi.

a) Kivumishi na kivumishi KKV → KV + KV

Mtoto mrefu mkubwa.

b) Kivumishi na kielezi KKV → KV + KL

Nguo nzuri kabisa.

c) Kivumishi na kirai- nomino. KKV → KV + KN

Tajiri mwenye duka kubwa amefariki

d) Kivumishi na kirai - kitenzi

KKV → KV + KT.

Kijana mwenye kufanya fujo atakamatwa na polisi

e) Kivumishi na kirai- kiunganishi.

KKV → KV + KKV

Mtoto mtovu wa nidhamu ameadhibiwa.

**Kirai- kiunganishi.**

Muundo wake hujikita kwenye mahusiano baina ya (kwa, na, katika au kwenye) na fungu la maneno linaloandamana nacho yaani kiria- kiunganish chenyewe. Neno kuu ni kiunganishi. Mfano;

Ameenda kwa baba yake

Ameweka katika chumba

Amezama kwenye pombe

**Vishazi (Vi).**

Dhana ya vishazi (kishazi).

Kishazi ni kundi la maneno lenye muundo wa kiima kiarifu hasa likiwa ndani ya sentensi kuu.

Miundo ya vishazi;

i) Huwa ni sehemu ya sentensi kuu: mfano;

- Baba amerudi lakini mama ameondoka.
- Kama atakuja, atatukuta hapa.

Katika sentensi hizi vishazi vemejumuishwa kwenye sentensi kuu kwa viunganishi au koma.vishazi hivyo ni; Baba anerudi. na Mama ameondoka.

ii) Vishazi hubebwa pia na vipashio ambavyo si sentensi (kama kirai-nomino). Mfano;

Kijana mdogo aliyeandikishwa shule jana ametoroka.

(KN) + (KT)

Kisima ambacho kimejaa tope tupu/ kimekauka.

(KN) + (KT)

Katika mifano hii virai nomino vina vishazi hivi: aliyeandikishwa shule jana na ambacho kimejaa tope tupu.

iii) Vishazi pia huweza kumilikiwa na virai vielezi. Mfano:

Wakati alipokuwa kijana nilimfahamu vyema.

**Aina za vishazi.**

a) Vishazi-viambatani.

b) Visahzi-vitegemezi.

**Vishazi viambatani.**

Vishazi viambatani huunganishwa katika sentensi kuu na viunganishi na koma.

Vikiondolewa kwenye sentensi kuu huwa vinajisimamia (huwa sentensi huru).Huwa na muundo wa kiima kiarifu.

- Huwa vina sifa sawa katika sentensi kuu vianamojitokeza. Mfano.

  Mama ameondoka lakini baba ameingia.

  Sentensi; Mama ameondoka. Baba ameingia, zina uzito sawa.

  Sentensi ifuatayo ni ambatani licha yakuwa ina vitenzi viwili tu.

  Walifika na wakampata.

**Vishazi tegemezi.**

Vishazi vitegemezi vikiondolewa kutoka sentensi kuu haviwezi kujisimamia.

Miundo ya vishazi tegemezi.

a) Miundo iliyojikita katika viambishi. Mfano:

Alipokuja tulifurahi.

Akinywa maji haya atadhurika.

Viambishi –po-, -ki-, nge-, -ngali,- ka-, ki, na –ye-, hutumika kama vishazi vitegemezi.

(b)Muundo uliyojikita katika neno au maneno. Mfano:

Ingawa alirudi kutoka Ulaya hakuwa na mali.

Ikiwa nitamwona nitakujulisha.

Kwa sababu ni tabia yake usimgombeze.

(c)Vishazi tegemezi hujikita katika udondoshaji wa vipashio. Mfano:

Hapendi kuonywa wala kushauriwa.

Baba ataamua kusema au kunyamaza.

Vishazi vitegemezi; kushauriwa na kusema katika mazingira ya sentensi hizi,vitenzi vinavyohusika haviwezi kurudiwa kwa hivyo hudondoshwa.

**Aina za sentensi katika lugha ya Kiswahili.**

Vigezo viwili vikuu hutumika katika kuainisha sentensi za Kiswahili:

a) Kigezo cha muundo
b) Kigezo cha maana

**Kigezo cha muundo**

Aina za sentensi kwa kutumia kigezo cha muundo;

a) Sentensi sahili.

b) Sentensi ambatani.

c) Sentensi changamano.

d) Sentensi tata.


**Sentensi sahili.**

Huwa ni kisahzi kimoja kinachojisimamia; huwa na muundo kiima na kiarifu na huleta maana kamili inayokusudiwa. Sentensi sahili huwa ya neno moja au sentenisi ya kisahzi kimoja. Mfano:

Anauza.(neno moja).

Mwalimu anafundisha. (kishazi kimoja).

Sentensi sahili inaweza kupambanuliwa kwa mtindo wa matawi ifuatavyo;




**Sentensi ambatani.**

- Huundwa kwa vishazi viwili au zaidi kwa kutumia viunganishi
- Vishazi vinavyounganishwa huwa vishazi huru.
- Miundo ya sentensi ambatano;

  a) Miundo yenye vishazi sahili tu.

- Ametibiwa sana lakini hajapona.
- Siogopi wala sitishiki.

b) Miundo yenye vishazi sahili na changamano. Mfano:

- Wanafunzi waliofika jana wamekwenda darasani lakini walimu wao hawakuwafundisha.

c) Miundo yenye vishazi changamano tu. Mfano:

- Mtoto aliyesimama pale barabarani ni wangu lakini yule aliyeketi ni wake.

d) Miundo yenye vishazi visivyounganishwa kwa viunganishi. Mfano:

- Mwambie aondoke.
- Waite wale.

**Kutambua tungo ambatano.**

Kuna njia mbalimbali za kutambua tungo ambatano;

Kutenganishwa na alama ya mkato (,) au semikoloni (;) Mfano:

- Simba aliyeingia zizini, ameua ng'ombe na mbuzi.

Tungo ambatano huwa na viunganishi; na, lakini, pia nk.
Mfano; Ingawa alikuwa na njaa aliamua kuacha chakula.

Hutumia vitenzi vinavyoshikilia kiambishi –ku- mfano;

- Aliyekuja <u>ku</u>imba ni ndugu yangu.

**Sentensi changamano.**

Huwa na kisahzi kikuu kimoja kinachojisimamia pamoja na kingine au vingine visaidisizi.

Ni sentensi iliyochanganyika na ina tungo sahili na tungo tegemezi kama kipashio chake kimojawapo au kama sehemu mojawapo yakipashio chake. Mfano;

- Aliyekuwa mwalimu mkuu wetu amepata uhamisho.

  Mtoto aliyeiba kalamu amehepa.

**Aina za sentensi kwa kutumia kigezo cha maana.**

a) **Sentensi sahili.**

Sentensi yenye ukamilifu wa maana. Pia hubeba wazo moja.
Mfano; Mtoto amelala.

b) **Sentensi tegemezi.**

Huhitaji kuegemezwa kwenye tunngo sahili ili maana yake ikamilike. Mfano.
Mtoto (aliyekuwa mgonjwa) amelala.

- Aliyekuwa mgonjwa ni sentensi tegemezi.

c) **Sentensi tata.**

Huwa na maana zaidi ya moja na maana zenyewe hazipo wazi kabisa. Kila maana ya sentensi tata huwa sawa. Mfano;
<u>Amepika mtoto</u>

i) Mtoto ametekeleza kitendo cha kupika

ii) Mtoto amepikwa na mtu mwingine

Sababu za kutokea utata:

i) Kukosa kuweka mkazo kwa neno linalohitajika. Mf:

- <u>Baba Juma</u> amefika.

- Baba <u>Juma amefika</u>

Maana mbili zinaweza kupatikana katika sentensi hii;

- Mtu anayeitwa Baba Juma.
- Au baba anajulishwa kwamba Juma amefika.

ii) Kutumia maneno yenye maana zaidi ya moja. Mf;

Aje Jumamosi.

- Jina la mtu.
- Inaleta maana ya siku.

iii) Utumiaji wa maneno kitaswira. Mfano;

Nina ua nyumbani.

Msichana mrembo.

Kitalu kinachozunguka nyumba.

iv) Mpangilio wa maneno katika sentensi. Mfano;

a) Mnyama ameua.

Mnyama ndiye aliyeua.

b) Ameua mnyama.

Mnyama aliuliwa na mtu fulani.

v) Utumiaji mbaya wa alama za uakifishaji.

**Kategoria amilfu za Kiswahili (vipashio vya sentensi ya Kiswahili).**

Habwe na Karanja (2007), anasema sintaksia huchunguza jinsi sentensi zinavyojengwa na kueleweka katika lugha mahususi.Katika muundo wa Kiswahili kuna sehemu mbili kuu;kiima na kiarifu.

**Kiima.**

Hii sehemu ya sentensi ambayo hukaliwa na jina/kikundi nomino.

Kiima ni mojawapo wa sehemu kuu ya sentensi nyingine ikiwa ni kiarifu- katika usemaji wa kawaida wa Kiswahili kiima hutangulia kiarifu.

Miundo tofauti ya kiima;

i) Nomino: Mzee amefariki.

ii) Nomino na nomino

Mwalimu Nyerere aling'atuka uongozini.

iii) Vikundi vya nomino na kivumishi

Kiongozi wetu amefika.

iv) Nomino na kimilikishi.

Mwalimu wetu mpole ataondoka.

**Kiarifu.**

Kiarifu ni sehemu ya sentensi ambayo kiini chake ni tendo lililotendwa.

Kiarifu huja baada ya kiima katika sentensi.

Miundo (vipashio) vya kiarifu;

i) Kitenzi kikuu

Mwalimu anafundisha

ii) Kitenzi/kitenzi kisaidizi + kitenzi kikuu

Mwalimu alikuwa anafundisha

alikuwa-kitenzi kisaidizi.

anafundisha-kitenzi kikuu.

iii) Kitenzi kishirikishi na shamirisho

Baba ni mpishi.

ni-kitenzi kishirikishi.

mpishi-shimirisho.

Mifano ya vitenzi vishirikishi; ni,si,yu,li,zi nk.

iv) Kitenzi kikuu na shamirisho na kielezi.

Mama amewachapa watoto vibaya sana.

amewchapa-kitenzi kikuu.

watoto-shamirisho.

vibaya na sana-kielezi(vielezi)

**Shamirisho.**

Hii ni nafasi katika sentensi ambayo hukaliwa na nomino au kikundi nomino kinachofuata kitenzi kikuu.

Shamirisho huwakilishwa mtendwa, mtendewa au kitendea. Mfano;

(a) Mama anapika chakula.

(b) Ali alimpiga mlinzi ngumi.

**Chagizo**

Nafasi katika mpangilio wa sentensi ambayo hukaliwa na vielezi vyote vya neno moja moja au kikundi kielezi au kielezi kishazi. Mfano:

(a) Walirauka alfajiri na mapema.

(b) Tuliwapata wakipanga kutoka.

**Maswali.**

1. Kwa kurejelea maoni ya wanaisimu watatu, eleza maana ya dhana ya sintaksia.

2. Eleza sababu zilizosababisha kuanzishwa kwa Sarufi Miundo Virai ukizingatia sifa zake kuu.

3. Andika sheria miundo virai za sentensi zifuatazo kisha uchore vielelezo vya matawi kuziwakilisha.

(a) Msichana mrembo alipika ugali kwa stovu.

(b) Mary wao aliimba wimbo mzuri.

(c) Susana alienda Kisumu kisha akaogelea katika ziwa Victoria.

4. Uktoa mifano kutoka Kiswahili eleza dhana zifuatzo kwa mujibu  Sarufi Mapokeo.

(a) kiima.

(b) kiarifu.

(b) shamirisho.

(c) chagizo.

5. Jadili aina mbalimbali za sentensi za Kiswahili.

6. Toa sababu za utata wa kimaana katika sentensi ya Kiswahili.

**Marejeleo.**

Habwe, J.na Karanja .P, 2007, Misingi ya Sarufi ya Kisdweahili. Nairobi.Phoenix Publishers.

Mdee,J.S. 1986: Kiswahili Muundo na Matunizi Yake. Nairobi. Intercontinental Publishers.

Kapinga,M.C. 1983: Sarufi Maunbo ya Kiswahili Sanifu.Dar es Salaam. TUKI.

Kihore,Y.M na wengine 2001:Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu.
Dar es Salaam. TUKI.

**Mfano wa mtihani wa chuo kikuu.**

**UNIT CODE: BEC 3102.** **UNIT TITLE: INTEGRATED KISWAHILI 1.**

**MAIN.EXAM** **TIME: 2HRS.**

---

**Jibu swali la kwanza na mengine yoyote mawili kutoka sehemu B .**

**SEHEMU YA A.**

1.(a) Fafanua dhana ya mofolojia. (alama 2)

(b) Eleza dhana zifutazo za kimofolojia. Toa mifano; (alama 6)

i) Leksimu

ii) Alomofu

iii) Mofu

(c) Jadili muundo wa kitenzi cha Kiswahili kwa kuzingatia umbo na viambishi, awali,kati na mwisho. (alama 4)

(d) Taja na ueleze matatizo mawili yanayokumba uainishaji wa ngeli kwa kuzingatia isebati na viambishi. (alama 4)

(e) Jadili kanuni mbili za kutambua mofimu. (alama 4)

(f) Fafanua sababu mbili zinzoleta utata katika sentensi ya Kiswahili. (alama 4)

(g) Nyumbua vitenzi vifuatavyo katika jinsi ya kufanyiza na kutendeka. (alama4)

La………………………….

Nywa………………………

(h) Tunga sentensi mbili ukitumia neno sana kama kielezi na kivumishi. (alama2)

**SEHEMU YA B.**

2. Jadili aina mbalimbali za sentensi za Kiswahili kwa kutumia kigezo cha muundo.Toa mfano na upambanue kila sentensi. (alama 20)

3. (a) Fafanua ngeli za Kiswahili kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi,tumia vitenzi kuonyesha upatanisho huo. (alama 10)

(b) Fafanua dhana ya kishazi na ujadili aina tatu za vishazi. (alama 10)

4. (a) Jadili aina mbalimbali za maneno ya Kiswahili.Toa mifano. (alama10)

(b) Kiswahili ni lugha ambishi, jadili muundo wa kitenzi cha Kiswahili kuthibitisha kauli hii. (alama 10)

5. Jadili dhana zifuatazo za muundo wa sentensi, toa mifano katika sentensi. (alama 20)

(a)kiima

(b)shamirisho

(c)chagizo.